



1 (800) 755-GROW (4769)
www.helpmegrow.org

Help Me Grow ni mfumo wa huduma za usaidizi kwa wanawake wajawazito, walezi walio na watoto wachanga na familia zilizo na watoto wadogo wenye matatizo ya kuchelewa kukua na ulemavu.



Department of
Health



Department of
Developmental
Disabilities

Je, wewe ni mjamzito au mlezi wa mtoto mchanga nyumbani?

Ziara za Nyumbani ni mpango wa kujitolea wa nyumbani unaotolewa bila malipo kwa familia. Wataalamu wa huduma ya ziara za nyumbani hutumia mbinu ya huruma ambayo inawawezesha wazazi kuwa na ujuzi, zana na ujasiri wa kuendeleza ukuaji bora wa mtoto katika miaka ya mapema zaidi - wakati muhimu zaidi wa ukuaji.

UNAWEZA KUTARAJIA NINI?

Wataalamu wa huduma ya ziara za nyumbani huunganisha wazazi na nyenzo zinazotoa msaada wa mahitaji ya msingi; hujibu maswali kuhusu ulezi na afya ya mtoto; na hutoa maeleo na kufanya uchunguzi ili kuendeleza ujauzito na maisha bora ya utotonii.

FAIDA ZA ZIARA ZA NYUMBANI:

Huduma ya Ziara za Nyumbani imethibitishwa kuboresha matokeo ya afya kwa wanawake wajawazito na watoto, kuimarisha uhusiano wa mzazi na mtoto na kukuza hali ya utayari wa kwenda shulenii.

Una wasiwasu kuhusu hali ya ukuaji wa mtoto? Chukua hatua mapema!

Huduma ya Msaada wa Mapema husaidia familia za watoto kuanzia wakati wa kuzaliwa hadi umri wa miaka mitatu wenye matatizo ya kuchelewa kukua au ulemavu ili wawe na mwanzo bora katika maisha. Ikiwa una wasiwasu kwamba huenda mtoto ana tatizo la kuchelewa kukua au ulemavu, ni muhimu uombe huduma za Msaada wa Mapema mapema iwezekanavyo.

UNAWEZA KUTARAJIA NINI?

Wataalamu wa huduma ya Msaada wa Mapema hushirikiana na familia ya mtoto ili kutambua uwezo na mahitaji na kushughulikia masuala ya ukuaji mapema iwezekanavyo. Huduma hizi hutolewa mahali ambapo familia huishi, huchenza na kukaa.

FAIDA ZA MSAADA WA MAPEMA:

Huduma ya Msaada wa Mapema inaweza kushughulikia aina zote za masuala ya ukuaji. Msaada wa mapema unaweza kupunguza hali ya kuhitaji huduma baadaye maishani.